

Afya yako ni muhimu kwa
kuhifadhi afya ya jamii

Wasiliana nasi



Ofisi
6800 78th Ave N, Brooklyn Park, MN
55445



Simu
763-307-4731



Facebook
<https://www.facebook.com/ACERFair>



Instagram
<https://www.instagram.com/acerfair/>



Majibu ya maswali yako ya Homa ya Mafua

Majibu ya baadhi ya maswali
ya kawaida na dhana potovu
kuhusu Homa ya Mafua



Je, Homa ya mafua ni nini?

Homa ya mafua ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vya mafua. Inaathiri mfumo wa kupumua wa mwili.

Dalili za mafua ni nini?

Dalili za kawaida ni Kuhisi baridi, joto ya mwili, kukohoa, kuumwa na koo, kutokwa na kamasi kwenye pua, kuumwa na kichwa, uchovu wa mwili na wakati mwingine kuhara.

Je, ninawezaje kuzuia kupata homa ya mafua?

Pata chanjo ya homa ya mafua, osha mikono yako mara kwa mara, funika pua na mdomo unapokohoa au kupiga chafya, epuka kugusa macho, pua au mdomo wako.

Kwa nini natakiwa kuchukua chanjo ya homa ya mafua kila mwaka?

Kinga ambayo chanjo ya mafua hutoa hupungua kwa muda. Chanjo za kila mwaka zinahitajika ili kudumisha ulinzi bora.

Je, mafua yanaweza kutibiwa?

Ukipata mafua, daktari anaweza kukupa dawa ya kuzuia makali ya virusi vya mafua ili kuitibu homa hii. Ni muhimu kutafuta matibabu kwa haraka ukipatwa na mafua.

*Maelezo kutoka kwa: <https://www.cdc.gov/flu/about/index.html>

Ukweli dhidi ya dhana potovu

Ukweli #1: Huwezi kupata homa ya mafua kutokana na chanjo

Chanjo dhidi ya homa ya mafua hutengenezwa kutoka kwa virusi ambavyo haviwezi kusambaza maambukizi. Kwa hivyo hakuna njia ya kupata homa kutoka kwa virusi.

Ukweli #2: Watu wenye afya njema wanahitaji chanjo ya homa ya mafua kwa ajili ya ulinzi pia

Watu wenye afya njema wanaweza kufaidika kwa kupewa chanjo. CDC inapendekeza watu wenye umri wa miezi sita na kuendelea kupata chanjo hii kila mwaka.

Ukweli #3: Wale ambao hawaonyeshi dalili za homa ya mafua wanaweza kuisambaza

Kati ya asilimia 20 na 30 ya watu wanaobeba virusi vya homa ya mafua wanaweza kueneza maradhi haya bila kuonyesha dalili zozote.

Ukweli #4: Homa ya Mafua haisababishwi na hali ya hewa kuwa baridi

Njia pekee ya kupata homa ya mafua ni kwa kuambikizwa na virusi vya mafua. Msimu wa homa ya mafua kwa kawaida unaambatana na msimu wa baridi.

Ukweli #5: Dawa aina ya antibiotics haziwezi kuponya dalili za homa ya mafua

Antibiotics hufanya kazi dhidi ya bakteria pekee. Hazitakuwa na ufanisi dhidi ya virusi vinavyosababisha homa ya mafua

*Maelezo kutoka: <https://www.health.harvard.edu/diseases-and-conditions/10-flu-myths>

Afya yako ni muhimu kwa
kuhifadhi afya ya jamii

Wasiliana nasi



Ofisi

6800 78th Ave N, Brooklyn Park, MN
55445



Simu

763-307-4731



Facebook

<https://www.facebook.com/ACERFair>



Instagram

<https://www.instagram.com/acerfair/>



Majibu ya maswali yako ya COVID-19 (UVIKO-19)

Majibu ya baadhi ya maswali ya
kawaida na hadithi potovu
kuhusu COVID-19



Diversity², LLC.

www.diversity2.org
info@diversity2.org
218-289-5566

COVID-19 ni nini?

COVID-19 ni ugonjwa unaosababishwa na aina mpya ya virusi vya Corona. Ina athiri mfumo wa kupumua (jinsi ya kupumua) wa mwili.

Dalili za COVID-19 ni zipi?

Baadhi ya dalili za COVID-19 ni kuhisi baridi au joto ya mwili, kukohoa, maumivu ya koo, pua kuvuja kamasi, maumivu ya mwili, maumivu ya kichwa, uchovu, kuhara, kupoteza hamu ya chakula, kupoteza hamu ya kunusa, na kupumua kwa shida.

Je, ninawezaje kuzuia kuambukizwa COVID-19?

Pata chanjo ya COVID-19 na unawe mikono yako mara kwa mara. Funika pua na mdomo wako unapokohoa au kupiga chafya. Epuka kugusa macho, pua au mdomo wako.

Ni kwa nini natakiwa kuchukua chanjo ya COVID -19?

Ulinzi ambao chanjo ya COVID-19 hutoa husaidia mwili kupigana na ugonjwa mbaya wa COVID-19. Chanjo ni salama kutumia na inakulinda.

Je, COVID-19 inaweza kutibiwa?

Ukiambukizwa COVID-19, tafuta usaidizi kutoka kwa daktari haraka uwezavyo. Daktari anaweza kukuuliza ulazwe hospitali kwa ajili ya matibabu.

*Maelezo Kutoka: <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-nCoV/index.html>

Ukweli dhidi ya dhana potovu

Ukweli #1 Chanjo haifanyi mtu awe na sumaku.

Chanjo haina kitu chochote ndani yake ambacho kinaweza kufanya uwe na sumaku. Kupata chanjo haitakufanya uwe sumaku. Chanjo zote za COVID-19(UVIKO-19) hazina aina yoyote ya chuma.

Ukweli #2: Chanjo haimwagi sehemu zake katika mwili wako

Chanjo za COVID-19(UVIKO-19) zinazopatikana Marekani hazina virusi vya moja kwa moja. Chanjo hazimwagi sehemu yoyote ndani au nje ya mili zetu. Chanjo hizi ni salama kutumia.

Ukweli #3: Chanjo ni salama kwa wanaolea mimba hivi sasa na wanaotumai kuwa wajawazito siku zijazo.

Hakuna uthibitisho unaoonyesha matokeo yasiyo salama kwa mimba au uzazi wakati wa kupewa chanjo. Ni salama kupokea chanjo ukiwa mja - mzito au unapanga kupata mtoto siku za usoni.

Ukweli #4: Chanjo za COVID-19 (UVIKO-19) hazibadilishi DNA yako

Chanjo ya COVID-19(UVIKO-19) hazibadilishi au kutangamana na DNA yako kwa njia yoyote. Hazina sehemu zozote ambazo zinaweza kubadilisha DNA. Chanjo hizi ni salama kutumia.

Ukweli #5: Chanjo hazisababishi mtu kupatikana na virusi vya COVID-19 anapopimwa.

Hakuna sehemu yoyote ya chanjo itakayokufanya upatikane na virusi vya COVID-19(UVIKO-19) unapopimwa. Chanjo hii ni salama, itakulinda wewe.

*Maelezo kutoka: <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/facts.html>